# Faharasa ya Mwongozo wa Familia

Faharasa hii ni orodha ya maneno ya kawaida ambayo hutumiwa katika elimu. Inajumuisha ufafanuzi rahisi na maelezo ya maneno ya kawaida kuhusu shule na elimu. Rasilimali hii itakusaidia kuelewa elimu ya mtoto wako vizuri.

## Mipango ya baada ya shule

Mipango ya baada ya shule ni shughuli ambazo hufanyika nje ya ratiba ya kawaida ya shule. Mipango hii imeundwa ili kuwasaidia wanafunzi kujifunza mambo mapya. Pia ni mahali pa wanafunzi kuburudika na kuwa salama wakati wazazi au walezi wao bado wako kazini. Baadhi ya mipango ya baada ya shule inaweza kujumuisha timu za michezo, mafunzo ya sanaa, masomo ya muziki, au mafundisho. Si lazima mtoto wako ashiriki katika mipango hii. Kushiriki ni kwa hiari.

## Mahudhurio

Mahudhurio yanamaanisha kwenda shuleni mara kwa mara. Mtoto wako anapaswa kwenda shuleni kila siku. Anapaswa tu kukosa kwenda shuleni akiwa mgonjwa au kwa sababu nyingine muhimu. Kwenda shuleni ni muhimu, ili aweze kujifunza na kuwa na marafiki. Mtoto wako anapokosa kwenda shuleni, anaweza kukosa kupata mafunzo kwa wakati unaofaa na kukosa kufanya shughuli za kufurahisha na wanafunzi wa darasa lake. Ili kujifunza zaidi, unaweza kutembelea Ukurasa wa Usaidizi wa Mahudhurio kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce).

## Mpango wa Elimu ya Ufundi wa Kazi (Career Technical Education (CTE))

CTE ni aina ya elimu ambayo huwasaidia wanafunzi kupata ujuzi na maarifa yanayoweza kuwatayarisha kwa kazi tofauti. Wanafunzi wanaweza kupata ujuzi na uzoefu katika masomo kama vile teknolojia, huduma za afya, uhandisi, na mengi zaidi. Ni njia ya wanafunzi ya kuchunguza machaguo tofauti ya kazi na kupata uzoefu muhimu ili kuwasaidia kufanikiwa katika siku zijazo.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

## Wanafunzi Wanaojifunza Lugha Mbili (DLL)

Katika mfumo wa utunzaji wa mapema na elimu, wanafunzi hawa hujifunza lugha mbili au zaidi kwa wakati mmoja kuanzia wanapozaliwa au huwa wanajifunza lugha ya pili baada ya kujifunza lugha yao ya kwanza. Maneno haya hutumiwa kurejelea wanafunzi ambao bado hawajaandikishwa katika shule ya chekechea. Wanapata ujuzi wa msingi wa lugha katika lugha yao ya kwanza pamoja na Kiingereza kama lugha ya pili au lugha mpya.

## Ngazi za elimu

Kuna ngazi tofauti za elimu ambazo wanafunzi hupitia. Kuna ngazi tano kuu: shule ya awali, shule ya msingi, shule ya kati, shule ya upili, na elimu ya baada ya sekondari. Unaweza kujifunza zaidi kwenye tovuti ya USA Hello.

### Shule ya awali

Shule ya awali ni shule ambayo watoto wadogo huenda kucheza na kujifunza kabla ya kuanza kuhudhuria shule ya chekechea. Kwa kawaida watoto huhudhuria shule ya awali wakiwa na umri wa kati ya miaka 3 na 5. Kuhudhuria shule ya awali huwasaidia watoto kuzoea utaratibu wa shule. Pia huwawezesha kujifunza na kujiunga na shughuli za kufurahisha na watoto wengine wenye umri wao. Katika umri huu, wanafunzi wanaweza kutambuliwa kama Wanafunzi Wanaojifunza Lugha mbili.

Wakati mwingine familia lazima zilipe ada ili mtoto wao aweze kuhudhuria shule ya awali. Kuna machaguo ya bure ya shule ya awali kwa familia zenye kipato cha chini kupitia mpango wa Kuwasaidia Watoto Maskini (Head Start program). Katika shule ya awali, watoto hujifunza jinsi ya kushiriki na watoto wengine na kujiandaa kwa shule ya chekechea. Shule ya awali pia ni wakati ambapo walimu na familia wanaweza kutambua mahitaji maalum ya kujifunza au ukuaji. Pamoja, familia na walimu wa shule ya awali wanaweza kusaidia katika kupata huduma ya afya, mafundisho, na usaidizi mwingine ambao utasaidia mahitaji maalum ya mtoto mdogo. Huko Ohio, Mpango wa Kuwasaidia Watoto Kukua (Help Me Grow program) hutoa usaidizi mwingi kwa familia zenye watoto wadogo.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

## Shule ya chekechea

Watoto huanza kuhudhuria shule ya umma na shule ya chekechea wakiwa na takriban umri wa miaka 5. Mafunzo ya shule ya chekechea yanaweza kuwa ya muda mfupi (nusu siku) au ya muda mrefu (siku nzima). Mafunzo ya shule ya chekechea ya nusu siku yanaweza kufanyika asubuhi au mchana. Muda ambao watoto hutumia katika mafunzo yao ya shule ya chekechea hutegemea wilaya ya shule.

## Shule ya Msingi

Watoto huhudhuria shule ya msingi kuanzia shule ya chekechea hadi darasa la tano. Wanafunzi wengi humaliza shule ya msingi wakiwa na umri wa miaka 10. Baada ya shule ya chekechea, huwa wanahudhuria darasa la kwanza katika mwaka unaofuata.

Kwa kawaida, watoto katika shule ya msingi hujifunza masomo tofauti kutoka kwa mwalimu mmoja katika darasa moja. Huwa wanajifunza kukuza ujuzi wa kuandika na hisabati na kujifunza kusoma, kufikiri kwa makini, na kutatua matatizo.

## Shule ya Kati

Katika shule ya kati, wanafunzi huwa na takriban umri wa miaka 11 hadi 13. Inaanza katika darasa la sita na kuishia katika darasa la nane. Kwa kawaida, wanafunzi wa shule ya kati huhudhuria madarasa tofauti kwa ajili ya masomo tofauti na huwa na walimu tofauti katika siku moja ya masomo.

## Shule ya Upili

Kwa kawaida wanafunzi huhudhuria shule ya upili wakiwa na umri wa miaka 14 hadi 18. Wanafunzi wengine wanaohitaji usaidizi mwingi zaidi wanaweza kuhudhuria shule ya upili hadi umri wa miaka 22.

Shule ya upili huanza katika darasa la tisa na kuishia katika darasa la 12. Madarasa hupangwa kulingana na masomo. Kwa kawaida mwanafunzi huwa na walimu tofauti siku nzima. Baadhi ya wanafunzi wanaweza kufanya kozi za kiwango cha juu na kujiandaa kwa ajili ya kazi au chuo. Wanafunzi wanaweza pia kuamua kuhudhuria Mpango wa Ufundi wa Kazi (Career Technical Education program) wa shule ya upili. Shule za upili pia huwa na vilabu, michezo, na shughuli nyingine.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

Katika shule ya upili, kila mwaka wa darasa huwa na jina:

- Kidato cha kwanza (darasa la 9).
- Kidato cha pili (darasa la 10).
- Kidato cha tatu (darasa la 11).
- Kidato cha nne (darasa la 12).

## Haki za Elimu

Haki za kiraia zimeundwa nchini Marekani ili kuhakikisha kuwa kila mtu ana fursa sawa na ulinzi wa kisheria, bila kujali mbari, dini, au sifa zao nyingine za kibinafsi. Baadhi ya mifano ya haki za kiraia ni haki ya kupata elimu ya umma, haki ya kupiga kura, kupata msaada kutoka kwa serikali, na haki ya kutumia maeneo ya umma. Haki za kiraia ni msingi wa haki ambazo wanafunzi na familia wanazo katika elimu.

Familia na wanafunzi wanaopokea usaidizi wa lugha ya Kiingereza wana haki. Hii inamaanisha kuwa unaweza kufanya maamuzi na kuchukua hatua ili kumsaidia mtoto wako kujifunza na kufaulu shuleni. Haki hizi ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wazazi na familia, kama yako, wanatendewa kwa haki na kwamba watoto wako wanapata elimu bora kadri iwezekanavyo.

## Uandikishaji

Uandikishaji ni unapomsajili mtoto wako ili aweze kwenda shuleni. Ni kama kujiunga na klabu au timu, lakini badala yake unajiunga na shule. Inamaanisha kuwa mtoto wako atakuwa mwanafunzi huko. Kila mtoto mwenye umri wa miaka 5 hadi 18 lazima aandikishwe shuleni.

## Mwanafunzi wa Kiingereza

Shule zinaweza kutumia maneno haya kwa wanafunzi wanaozungumza lugha zaidi ya moja na walio na alama za mtihani wa Kiingereza za kiwango cha chini cha ustadi katika kusoma, kuandika, au kuzungumza. Wanafunzi hawa huandikishwa shuleni na hupata mafundisho na usaidizi mwingine wa kujifunza kuzungumza, kusoma, kuandika, na kuelewa Kiingereza. Kwa kwaida, wanafunzi ambao ni wanafunzi wa Kiingereza huzungumza lugha moja au zaidi ambayo si Kiingereza nyumbani.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

## Usaidizi wa lugha ya Kiingereza (msaada wa ziada ili kukuza ujuzi wa Kiingereza)

Kila shule inapaswa kutoa msaada wa ziada kwa wanafunzi wanaohitaji kukuza ujuzi wao wa Kiingereza. Kila shule inaweza kufundisha Kiingereza kwa njia tofauti. Kila mwaka, mtoto wako atafanya mtihani (Tathmini ya Lugha ya Kiingereza ya Ohio) ili tujue ujuzi wake wa lugha ya Kiingereza. Mtoto wako atapata usaidizi wa lugha ya Kiingereza hadi atakapopita mtihani.

Usaidizi wa lugha ya Kiingereza unaweza kujumuisha:

- Mafunzo ya kuwasaidia wanafunzi kujifunza Kiingereza.
- Msaada wa ziada wakati wa mafunzo ya kawaida, kama sayansi au hisabati, ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa mambo wanayojifunza.

## Ustadi wa Lugha ya Kiingereza

Ustadi wa lugha ya Kiingereza unamaanisha kuwa na uwezo wa kuzungumza, kuelewa, kusoma, na kuandika Kiingereza vizuri sana. Shule hutumia mitihani (kama vile Tathmini ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio) ili kuangalia jinsi wanafunzi wanavyotumia Kiingereza. Kuwa na ustadi kunachukua muda na kunahitaji mazoezi. Mtu anapokuwa na ustadi wa lugha ya Kiingereza, anaweza kuwasiliana vizuri kwa lugha ya Kiingereza (kuzungumza, kusoma, kuandika, na kuelewa).

## Shughuli za Baada ya Masomo

Shughuli za baada ya masomo ni shughuli ambazo mtoto wako anaweza kujiunga nazo baada ya siku yake ya kawaida ya masomo. Shughuli hizi zinaweza kuwa michezo, muziki, vilabu, au kujitolea. Zinaweza kumsaidia mtoto wako kupata marafiki wapya, kujifunza ujuzi mpya, na kufurahia. Hii pia ni njia nzuri ya kuwa mtendaji na kuwa na afya njema.

## Mwasiliani wa Familia

Mwasiliani wa familia ni mtu anayeweza kuzungumza lugha zaidi ya moja na kusaidia familia na shule kushirikiana. Huwa anashirikiana na wazazi, walimu, na shule ili

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

kuhakikisha kuwa wahusika wote wanaelewana. Hii huwasaidia wanafunzi kufanya vizuri zaidi shuleni.

## Msaada wa Kifedha

Msaada wa kifedha wa wanafunzi nchini Marekani ni pesa ambazo wanafunzi wanaweza kupata ili ziwasaidie kulipia elimu baada ya shule ya upili kama chuo au elimu ya ufundi wa kazi. Pesa hizi zinaweza kutoka kwa serikali, shule, na vikundi vya kibinafsi. Zinaweza kutolewa kama ruzuku, mkopo, ajira ya kujifunza kazi, au ufadhili wa masomo. Ili wanafunzi waweze kuomba msaada wa shirikisho, wanahitaji kujaza Maombi ya Bure ya Msaada wa Wanafunzi wa Shirikisho (Free Application for Federal Student Aid (FAFSA)).

## Chakula cha Bure na cha Bei Iliyopunguzwa

Chakula cha bure na cha bei iliyopunguzwa ni chakula ambacho wanafunzi wanaweza kupata shuleni kwa gharama kidogo au bila gharama. Familia zenye kipato cha chini zinaweza kustahiki kwa vyakula hivi na zinaweza kutuma maombi ili ziweze kuvipata. Mpango wa Idara ya Elimu ya Marekani (US Department of Education) hupatia kila jimbo fedha za kuwasaidia kulipia vyakula hivi na usaidizi mwingine kwa familia zeneye kipato cha chini.

## Elimu kwa Wanafunzi wenye Kipaji

Elimu kwa wanfunzi wenye kipaji inamaanisha kutoa madarasa au mipango maalum kwa wanafunzi wenye kipaji katika masomo fulani. Madarasa haya huwapa wanafunzi nafasi ya kujifunza zaidi na kutatua matatizo yanayolingana na uwezo wao.

## Alama

Hizi ni alama ambazo walimu huwapa wanafunzi kwa ajili ya kazi wanazofanya darasani. Huwa zinaonyesha jinsi mtoto wako anavyoelewa na kukamilisha kazi. Zinaweza kutumiwa kufuatilia maendeleo ya mtoto wako katika mwaka wa masomo. Kwa kawaida, alama za juu humaanisha utendaji bora. Alama duni zinaweza kuonyesha nyanja ambazo huenda mtoto wako akahitaji kuboresha.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

## Mafundisho ya Nyumbani (Kujifunza nyumbani)

Huko Ohio, wazazi wanaweza kuamua kuwaelimisha watoto wao nyumbani badala ya kuwapeleka shuleni. Wanahitaji tu kumwambia msimamizi mkuu wa wilaya ya shule wa eneo lao na kufuata sheria za Ohio za mafundisho ya nyumbani. Jifunze zaidi kwenye ukurasa wa Mafundisho ya Nyumbani wa tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce).

## Utafiti wa Lugha ya Nyumbani (Utafiti wa Lugha Inayotumiwa)

Utafiti wa Lugha Inayotumiwa ni fomu ambayo shule hutumia kujifunza kuhusu lugha ambazo familia huzungumza nyumbani. Familia zinaweza kutumia fomu hii kushiriki lugha ambayo zinapendelea kutumia. Shule inapaswa kutumia taarifa kutoka kwa fomu hii ili kushiriki taarifa na familia katika lugha wanayopendelea kutumia. Wanafunzi wa familia ambazo hutumia lugha nyingine ambayo si Kiingereza nyumbani wanaweza kuhitaji kuangalia ikiwa mwanafunzi anahitaji msaada wa ziada ili kukuza ujuzi wake wa Kiingereza.

## Ukalimani (au Tafsiri)

Ukalimani, au tafsiri, inamaanisha kuchukua maneno au sentensi kutoka katika lugha moja na kuyaandika au kuyazungumza katika lugha nyingine. Hii huwasaidia watu wanaozungumza lugha tofauti kuelewana vizuri zaidi.

## Mkalimani (au Mtafsiri)

Mkalimani au mtafsiri ni mtu ambaye hubadilisha maneno mtu amesema au kuandika katika lugha moja hadi lugha nyingine. Hii huwasaidia watu wanaozungumza lugha tofauti kuelewana.

## Afya ya Akili

Ni muhimu kutunza akili zetu kama tu vile tunavyotunza miili yetu. Afya ya akili inahusu jinsi tunavyohisi na kufikiri. Inajumuisha hisia, tabia, na njia za kujifunza. Watoto wanapokuwa na afya njema ya akili, wanaweza kuhisi furaha na kujiamini. Wanaweza pia kufanya vizuri shuleni na kuwa na mahusiano mazuri na familia na marafiki.

## Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce)

Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce) husimamia shule zinazofundisha watoto huko Ohio. Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio ni shirika la watu wanaoshirikiana ili kusaidia shule na walimu kuhakikisha kuwa watoto wanajifunza na kukua. Huwa wanatunga sheria na kutoa mwongozo wa kusaidia shule kuwa bora zaidi.

## Tathmini ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio (Ohio English Language Proficiency Assessment (OELPA))

Tathmini ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio ni mtihani unaofanywa na wanafunzi wanaochukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza. Mtihani huu huwasaidia walimu kuelewa jinsi wanafunzi wanaweza kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika kwa Kiingereza. Pia huwasaidia walimu kujua jinsi wanavyoweza kuboresha ujuzi wao wa lugha. Mtihani huu ni muhimu kwa wanafunzi wanaohitaji msaada wa ziada wa kujifunza Kiingereza ili waweze kufaulu shuleni na baada ya shule. Kila wakati wanafunzi wanapofanya mtihani huu lazima shule ishiriki matokeo na familia.

### Tathmini Mbadala ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio (Alternate Ohio English Language Proficiency Assessment (Alt-OELPA))

Alt-OELPA ni mtihani ambao hupima jinsi wanafunzi wa Kiingereza wa madarasa ya Chekechea-12, walio na matatizo makubwa ya utambuzi wa kiakili, wanaweza kuelewa na kutumia lugha ya Kiingereza. Mtihani huu hupima ujuzi wao wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika na unajumuisha lugha ya Kiingereza wanayohitaji ili wawze kufanya kazi zao za shule. Alt-OELPA huwapa wanafunzi hawa fursa ya kuonyesha kile wanachojua kwenye mtihani unaozingatia matarajio tofauti ya kujifunza Kiingereza. Unaweza kutembelea ukurasa wa Alt-OELPA wa tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education).

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

## Mtihani wa Ustadi wa Lugha ya Kiingereza wa Ohio (Ohio English Language Proficiency Screener (OELPS)

OELPA ni mtihani ambao shule hutumia kubainisha ikiwa mwanafunzi anachukuliwa kuwa mwanafunzi wa Kiingereza na ikiwa anahitaji msaada wa kujifunza Kiingereza. Kwa kawaida, wanafunzi hufanya mtihani huu baada ya familia yao kufanya Utafiti wa Lugha Inayotumiwa au shule ikigundua kuwa familia ya mwanafunzi hutumia lugha nyingine ambayo si Kiingereza nyumbani.

## Wilaya ya Shule

Wilaya ya shule ni kikundi cha shule za eneo moja. Zinashirikiana ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wa eneo lao wanaweza kuhudhuria shule nzuri. Kila wilaya ya shule ina sheria na viongozi wake ambao hufanya maamuzi ya shule zote katika wilaya.

## Elimu Maalum

Mipango ya elimu maalum huwapa wanafunzi usaidizi ikiwa wana ulemavu wa kimwili, kiakili, au ulemavu mwingine. Huenda wanafunzi wanaohitaji elimu maalum wana shida ya kujifunza katika darasa la kawaida. Wanaweza kupata msaada katika darasa tofauti. Hii ni kwa ajili ya kuwasaidia kufaulu katika elimu yao. Hii huwasaidia kujifunza kwa njia inayowafaa.

## Kambi ya Majira ya Joto

Kambi ya majira ya joto ni mahali ambapo watoto huenda wakati wa mapumziko yao ya majira ya joto kutoka shuleni. Huwa wanapata fursa ya kufanya shughuli za kufurahisha kama vile spoti, sanaa na ufundi, na michezo. Huwa wanapata pia fursa ya kuwa na marafiki wapya. Wanaweza kujifunza mambo mapya katika mazingira salama na yanayosimamiwa.

## Chuo Kikuu (au Chuo)

Chuo kikuu au chuo ni mahali ambapo wanafunzi huhudhuria ili kuendeleza masomo baada ya kumaliza shule ya upili. Huwa wanafanya mafunzo ili wajiandae kwa kazi ambazo wangependa kuwa nazo katika siku zijazo. Vyuo vikuu ni vikubwa kuliko shule

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

za upili na vina majengo mengi ya wanafunzi, kama madarasa, maktaba, na mabweni.

## Mafundisho ya Mtandaoni (au Kujifunza Ukiwa Mbali au Mtandaoni)

Mafundisho ya mtandaoni ni wakati ambapo wanafunzi hutumia teknolojia kama vile kompyuta na intaneti kujifunza. Wanafunzi hufanya mafundisho ya mtandaoni wanapojifunza na kukamilisha kazi mtandaoni. Mafundisho ya mtandaoni yanaweza kufanywa shuleni, nyumbani, katika maktaba, au maeneo mengine katika jamii.

## Mafunzo ya Kazi (au Elimu ya Ufundi wa Kazi)

Mafunzo ya kazi ni aina nyingine ya mpango wa elimu ambao wanafunzi wanaweza kushiriki wakiwa katika shule ya upili. Mipango hii kwa kawaida hulenga kuwafundisha wanafunzi kuchagua kazi au biashara mahususi, kama vile kuunganisha chuma, usalama, kilimo, ukaribishaji wageni, ujenzi, au huduma ya afya. Wanafunzi wanaoshiriki katika mipango hii wanaweza pia kujifunza ujuzi mahususi kama vile jinsi ya kukarabati kompyuta au kupika.

*Rasilimali hizi zinalenga kuimarisha masomo, ustawi wa wanafunzi, na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa Ohio wanaozungumza lugha nyingi. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi za kushirikiana kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce) na Kituo cha Chuo Kikuu cha Jimbo la Ohio cha Elimu na Mafunzo ya Kazi (The Ohio State University's Center on Education and Training for Employment) pamoja na kikundi cha kujitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 